ISSN 0856 - 0323

MWAKA WA 82
TOLEO NA. 49

7 Desemba, 2001

# GAZETI

BEI SH. 200/=

## LA

DAR ES SALAAM

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Linatolewa kwa Idhini ya Serikali na Kuandikishwa Posta kama Gazeti**

## YALIYOMO

| | Taarifa ya Kawaida | Uk. |
|---|---|---|
| Notice *re* Supplement | Na. 806 | 1015/16 |
| Tanzia | | 1016/19 |
| Kupotea kwa Hati za Kumiliki Ardhi | Na. 807-11 | 1019/20 |
| Uchunguzi wa Migogoro ya Kikazi | Na. 812-4 | 1020/8 |
| Uthibitisho na Usimamizi wa Mirathi | Na. 815 | 1028 |

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 806

Notice is hereby given that Sheria Ndogo. By laws and Order as set out below. have been issued and are published in Subsidiary Legislation Supplement No. 45 dated 7th December. 2001 to this number of the *Gazette:—*

Sheria Ndogo za (Mifugo) za Halmashauri ya Wilaya ya Nzega (Tangazo la Serikali Na. 432 la 2001).

Sheria Ndogo za (Mahudhurio ya Wanafunzi wa shule ya Msingi na Sekondari za Serikali) 2001. za Halmashauri ya Wilaya ya Nzega (Tangazo la Serikali Na. 433 la 2001).

Sheria Ndogo za (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Nzega 2001 (Tangazo la Serikali Na. 434 la 2001).

The Nzega District Council (Cultivation of Agricultural Land) By laws 2001. (Government Notice No. 435 of 2001).

The Mwanza Municipal Council (Service Levy) By laws. 2001 (Government Notice No. 436 of 2001).

Sheria Ndogo za (Kodi ya Maendeleo) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (Tangazo la Serikali Na. 437 la 2001).

Sheria Ndogo za (Upandaji Miti na Kuhifadhi Misitu) (marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (Tangazo la Serikali Na. 438 la 2001).

Sheria Ndogo za (Ushuru wa Majengo) za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (Marekebisho) 2001 (Tangazo la Serikali Na. 439 la 2001).

Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mifugo) (Marekebisho) za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, 2001 (Tangazo la Serikali Na. 440 la 2001).

Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (Ada ya Mikokoteni) Sheria Ndogo za mwaka 2001 (Tangazo la Serikali Na. 441 la 2001).

Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, (Ushuru wa Mazao ya Misitu) za 2001 (Tangazo la Serikali Na. 442 la 2001).

Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (Ada ya shughuli za Kiutamaduni) 2001 (Tangazo la Serikali Na. 443 la 2001).

Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga) (Marekebisho) 2001 (Tangazo la Serikali Na. 444 la 2001).

Matangazo yahusuyo mali za watu waliofariki. kuvunja mikataba ya ushirikiano na mengineyo. yakiwa ya manufaa kwa umma yaweza kuchapishwa katika *Gazeti.* Yapelekwe kwa **Mhariri, Idara Kuu ya Utumishi—Ofisi ya Rais, S.L.P. 2483, Dar es Salaam, Simu za Ofisi 118531/4.** Kabla ya *Jumamosi ya kila Juma.*

Limepigwa Chapa na Mpigachapa wa Serikali. Dar es Salaam – Tanzania

Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (Ushuru wa Kusafisha na kupitisha mifugo)za mwaka 2001 (Tangazo la Serikali Na. 445 la 2001).
Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Ada za Vileo (Pombe za Kienyeji) za 2001 (Tangazo la Serikali Na. 446 la 2001).
Sheria Ndogo za (Ushuru wa Baiskeli) za Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga (Marekebisho) 2001 (Tangazo la Serikali Na. 447 la 2001).
Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi (Ushuru wa Mifugo na Ada ya Kibali cha kusafirisha mifugo) ya mwaka 2001 (Tangazo la Serikali Na. 448 la 2001).
Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi (Kodi ya Maendeleo) za 2001. (Tangazo la Serikali Na. 449 la 2001).
Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi (Ada na Ushuru) za mwaka 2001 (Tangazo la Serikali Na. 450 la 2001).
Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi Uchuuzi na Biashara Ndogo Ndogo za Mitaani za mwaka 2001 , (Tangazo la Serikali Na. 451 la 2001).
Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi (Ada za Shughuli za Kitamaduni) za mwaka 2001. (Tangazo la Serikali Na. 452 la 2001).
The Shinyanga District Council (Guest House and Lodging Fees) By laws, 2001 (Government Notice No. 453 of 2001).
The Shinyanga District Council (Service Levy) By laws, 2001 (Government Notice No. 454 of 2001).
Order under the University of Dar es Salaam Act. 1970 (Government Notice No. 455 of 2001).
Order under the Water Works Ordinance (Government Notice No. 456 of 2001).

## TANZIA

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na D. 3677 PC James Matembe aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 23/6/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. D. 3167 PC Thomas Masondo Kindole aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 27/6/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na EX.D. 755 PC John Mwakisumbwe aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 28/6/2001

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. E. 55 PC Joseph Ochang'a aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 17/11/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. D. 8288 PC Joseph Kapufi Ntindi aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 16/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. E. 1522 PC John Mtonyi aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 19/7/2001

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. D. 6115 PC Bwire Mukali aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 24/6/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. E. 6041 PC Cosmas Josephat aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 1/6/2001

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. WP. 1075 SGT Sophia Komba aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 21/6/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. E. 8400 PC Robert B. Mwaipungu aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 5/5/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. D. 6367 CPL Jonathan Mgema aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 3/6/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. A. CPL Ngeta aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 4/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. C. 1790 D/CPL Waziri Makata aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 19/8/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na Z. 2314 S/SGT Lucas Vicent aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 18/6/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. WP. 4084 PC Stella Francis aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 11/6/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. WP. 2955 PC Martha Chuma aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 20/7/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. EX. 6361 Emmanuel Komba aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 17/7/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. E. 7833 PC Aminiel Mkwama aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 14/6/2001

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. B. 9731 SGT Materine Gulukota aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 30/6/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. E. 5817 PC Thomas Raphael aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 14/6/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. C. 3993 SGT Athuman Mangu aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 18/7/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. E. 6824 PC Theofred aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 2/1/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. E. 6039 PC Kimweti Marika aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 17/7/2001

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. C. 1521 SGT Mohamed Njujiro aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 20/6/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. D. 7836 PC Stephen Marcus aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 9/6/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. WP. 1239 PC Mary Mwaluanda aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 23/1/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. WP. 3092 PC Prisca Joseph aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 19/5/2001

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. 2626 SGT Helena Kamsofi aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 29/6/2001

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. 9819 S/SGT Issa Mtoro aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 18/6/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. US. 12493 ASP Paschal Joseph Ndekero aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 24/6/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. A. 8098 WDR Joram aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 27/6/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. A. 5490 CPL Fidelis Nyulahe aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 3/6/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. A. 8468 WDR Alexander Patrick aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 28/6/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha Ndugu Miheli Nkembo - M/O.1 aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 21/6/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. A 9376 SGT Egon Bidirigi aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 30/6/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. E. 1034 PC Saidi Shaha Mtonga aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 5/6/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. WP. 2046 PC Mwanaidi Shaaban aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 14/6/2001

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. WP. 3295 3295 PC Nindael aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 4/6/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. D. 5011 CPL Hassan Vuaa aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 11/8/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. A. 5159 CPL Benny Mwakalinga aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 1/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. A. 8960 WDR Salum H. Amri aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 4/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. A. 7123 CPL Philipo M. Mtunya aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 24/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. A. 6545 CPL Juma Saidi Ilinda aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 23/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha Ndugu Lucy N. Poñela - MO/MWD II aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 21/7/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. PF. 1377 INSP. Amir Ibrahim Mkumbi aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 2/7/2001

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. C. 8313 CPL Mutashobya Mussa aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 4/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. A. 8526 WDR Thomas Gaudence Masawe aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 23/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. WP. 958 D/CPL Asha Omar aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 19/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha Ndugu Fredrick Onanda - Acct. II aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 31/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. D. 2297 PC Gamba Majogolo aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 18/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. D. 1279 PC Yose Anthony aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 20/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. Z. 2014 PC Mustafa Yusufu Hamisi aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 16/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. E. 4271 PC Kacob Maganga aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 22/7/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. C. 818 SGT Mohamed mrope aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 23/7/2001.

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na.A. 7790 WDR Leonard Y. Nachunga aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 8/8/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. D. 2208 PC Emmanuel Stephano aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 2/8/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. B. 7651 S/SGT Charles Hassan aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 22/8/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. D. 9173 CPL Nasoro Mbarouk aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 17/8/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. D. 4494 PC Charles Mwesigwa aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 18/8/2001.

---

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anasikitika kutangaza kifo cha askari Na. 1411 PC Stanley Mlawa aliyekuwa mtumishi wa Wizara ya Mambo ya Ndani kilichotokea tarehe 23/8/2001.

---

Taarifa ya Kawaida Na. 807

## KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

*Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi*

(Sura 334)

*Hati Nambari:* 26486.

*Mmiliki aliyeandikishwa:* Francis Mwanangwa Mlozi.

*Ardhi:* Kiwanja Na. 126 Low Density area, Msasani Vilage, Jijini Dar es Salaam.

*Mwombaji:* Caroline Francis Mlozi.

Taarifa Imetolewa kwamba Hati ya Kumiliki Ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

Hati ya Asili ikionekana, lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati, S.L.P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
4 Novemba, 2001

T. S. Mwakilema,
*Msajili wa Hati*

---

Taarifa ya Kawaida Na. 808

## KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

*Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi*

(Sura 334)

*Hati Nambari:* 32899.

*Mmiliki aliyeandikishwa:* Josephine Kabika.

*Ardhi:* Kiwanja Na. 29 kitalu '19' Mwananyamala, Jijini Dar es Salaam.

*Mwombaji:* CRDB Bank Limited

Taarifa Imetolewa kwamba Hati ya Kumiliki Ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

Hati ya Asili ikionekana, lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati, S.L.P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
19 Juni, 2001

T. S. Mwakilema,
*Msajili wa Hati*

---

Taarifa ya Kawaida Na. 809

## KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

*Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi*

(Sura 334)

*Hati Nambari:* 45169

*Mmiliki aliyeandikishwa:* The Registered Trustees of the Apostolic church Tanzania

*Ardhi:* Kiwanja Na. 581 Kitalu '10' Mwananyamala, Jijini Dar es Salaam.

*Mwombaji:*

Taarifa Imetolewa kwamba Hati ya Kumiliki Ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

Hati ya Asili ikionekana, lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati, S.L.P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam,
5 Desemba, 2001

Subira Sinda
*Msajili wa Hati*
*Msaidizi Mwandamizi*

---

Taarifa ya Kawaida Na. 810

## KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI

*Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi*

(Sura 334)

*Hati Nambari:* 186071/29/28.

*Mmiliki aliyeandikishwa:* transcontinental Trading Company Limited.

*Ardhi:* Kiwanja Na. 164 Pugu Road, Jijini Dar es Salaam.

*Mwombaji:* Transcontinental Trading Company Limited.

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya Kumiliki Ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana, lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati, S.L.P. 1191, Dar es Salaam.

Dar es Salaam, T. S. MWAKILEMA,
28 Novemba, 2001 *Msajili wa Hati*

---

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 811

KUPOTEA KWA HATI YA KUMILIKI ARDHI
*Sheria ya Uandikishaji wa Ardhi*
(Sura 334)

*Hati Nambari:* 38536
*Mmiliki aliyeandikishwa:* MANZOOR PANJU JESSA.
*Ardhi:* Kiwanja Na. 369 Jangwani Beach, Jijini Dar es Salaam.
*Mwombaji:-*

TAARIFA IMETOLEWA kwamba Hati ya Kumiliki Ardhi iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa Hati mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa miezi miwili tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

HATI YA ASILI ikionekana, lazima irudishwe kwa Msajili wa Hati. S.L.P. 1191. Dar es Salaam.

Dar es Salaam. T. S. MWAKILEMA,
5 Desemba, 2001 *Msajili wa Hati*

---

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 812

MGOGORO WA KIKAZI
baina ya
S. Z. CHAPA NA WENZAKE - TANGA
na
MAMLAKA YA BANDARI - DAR ES SALAAM

UAMUZI WA HOJA ZA AWALI

William - DC

Huu ni mgogoro wa uchunguzi kati ya S. Z. Chapa na wenzake (ambapo hawakuwakilishwa) kama walalamikaji na mwajiri wao Mamlaka ya Bandari ambaye aliwakilishwa na Msomi Wakili Mchome.

Kabla ya mgogoro huu wa uchunguzi haujaanza kusikilizwa, Msomi Wakili Bw. Mchome kwa niaba ya mwajiri alitoa pingamizi la kisheria. Mahakama baada ya maelezo ya pande zote mbili kuhusiana na pingamizi hilo ilitolea uamuzi mfupi juu ya kutokuwepo washauri. Mahakama ilijipeleka katika kifungu cha 28 cha Sheria Na. 41 ya 1967 kama ilivyorekebishwa, na kuweza kuendelea kusikiliza pingamizi za awali bila ya Washauri. Ingaw shauri hili halihusiki na sheria 2/2000 kwa vile lilifunguliw kabla, lakini mahakama ilitumia kifungu tajwa hapo juu n kuamua kuwa iendelee kwenye pingamizi bila Washauri kw vile majina ya washauri huwa yanacheleweshwa kuletwa n Waziri. Pia mahakama iliona kuna umuhimu wa kufanya hivyo baada ya kuona kuwa Walalamikaji wanatoka Tanga na walipunguzwa kazi toka mwaka 1994 ingawa shauri lilifunguliwa mwaka 1999.

Nikizingatia hayo uamuzi utakuwa wangu peke yangu. Msomi Wakili Bw. mchome alitoa pingamizi la kisheria kuwa mgogoro huu ni batili kwa vile umeletwa na Walalamikaji bila ya kukidhi matakwa ya fungu la 67 (a) la sheria iliyoanzisha mamlaka ya Bandari (Tanzania Harbours Authority) 1967. alisema Bw. Mchome kuwa Walalamikaji walitakiwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja kwa mamlaka kabla ya kufungua shauri hili. Akielezea hoja yake hiyo Msomi wakili Bw. Mchome alisema kuwa taratibu hizo za kisheria zinamtaka mtu anayekusudia kuanzisha shauri au madai dhidi ya mamlaka, anapaswa atoe taarifa ya siku 30.

Msomi wakili Bw. mchome akifafanua zaidi ju a pingamizi hili alisema kuwa kifungu cha 67 kinamtaka mtu/ watu hao watoe taarifa ikionyesha madai yanayokusudiwa kufunguliwa na matakwa yake pia.

Akitoa tafsiri zaidi alisema kuwa Bodi ndiyo iliyokuwa na mamlaka ya kupunguza au kuachisha kazi au kuajiri na kuwa Bodi hiyo inatawaliwa na sheria ya Mamlaka ya Bandari na ndiyo inayotekeleza, hivyo walalamikaji alisema, walitakiwa wafuate sheria inayotawala mamlaka kwa kuleta madai yao mahakamani.

Msomi Wakili Bw. Mchome alieleza kuwa matakwa hayo kwa vile hayakutekelezwa basi aliomba mahakama hii itupilie mbali madai haya.

Pili, msomi wakili Bw. Mchome alitoa hoja, kwamba madai hayo yako nje ya muda uliowekwa na sheria, alisema kuwa kifungu 67(b) madai yalitakiwa yaletwe ndani ya n i 12 katika mahakama. Akielezea kuhusu shauri hili kuwa limeletwa nje ya muda na kusema kuwa zoezi la kuwapunguza kazi lilifanyika 1994/95 wakati hawa walalamikaji wameleta madai yao 1999 na kusema ingawa haikuonyesha wazi kwenye malalamiko yao.

Msomi Wakili alitaka mahakama ipokee kesi kati ya *Mary Gagriel & Other Vs Tanzania Harbours Authority* civil Case No. 337/99 HC Dsm (unreported) ambapo mahakama ilitupilia mbali madai yake kwa kuletwa nje ya muda. Katika hali hiyo, alisisitiza kuwa hatua ya kuwasilisha mgogoro huu mbele ya mahakama ya kazi baada ya muda kupita ni kukiuka taratibu zilizowekwa. Hivyo Bwana Mchome alitoa rai kuwa kutokana na ukiukwaji wa sheria na kanuni katika uwasilishaji wa mgogoro huu hivyo aliomba utupiliwe mbali.

Jambo la tatu, alisema msomi wakili Bw. Mchome ni kuwa Mamlaka ya Bandari ilikuwa specified chini ya GN 543/97 na pia chini ya Sheria ya ufilisi Cap. 25 Section 9 hivyo kwa

Walalamikaji walitakiwa wapate ridhaa ya Mahakama Kuu kufungua shauri hili. Pia alisisitiza kusema kuwa kwa vile hakuna kibali cha Mahakama Kuu basi shauri hili litupiliwe mbali.

Jambo la nne, alisema Msomi Wakili Bw. Mchome kuwa baada ya Mamlaka ya Bandari kuwa specified chini GN 543/97 na kuwa chini ya PSRC Walalamikaji walitakiwa washtaki PSRC na siyo Mamlaka ya Bandari. Bw. Mchome aliitaka mahakama hii ipitie kesi ya OTTU *Kny. Wafanyakazi Kilimanjaro Hotel Ltd. Vs Kilimanjaro Hotel Ltd.*

Civil Case No. 45/97 (unreported) Mh. J.C. Msumi, alitupilia mbali kwa vile aliyetakiwa kushtakiwa ni PSRC na siyo Kilimanjaro Hotel.

Katika kuijadili hoja hii Bw. Mchome Wakili alieleza kuwa Mamlaka ya Bandari hawana "Cause of action" kwa vile walisha binafsishwa chini ya Tangazo Na. 543/97 na hivyo kuomba rai kuwa mahakama hii pia itupilie mbali shauri hili.

Akipinga hoja hizo za Msomi Wakili Bw. Mchome, Bw. Chapa mwakilishi wa wenzake alitoa sababu za kupinga hoja hizo. Kwanza alisema kuwa kifungu cha 67 (a) cha sheria ya Mamlaka ya Bandari hakihusiki na shauri hili kwa vile shauri hili linalohusika na limeletwa chini ya Sheria ya Kazi 1967 kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 2/93 chini ya kifungu 8(a).

Bw. Chapa alieleza kuwa walifuata taratibu zote kuanzia kwenye tawi kazini kwao na kumjulisha pia mwajiri wao, ambaye hakukubaliana na malalamiko yao.

Kwa kumalizia kujibu hoja ya kwanza Bw. Chapa alisema kuwa yeye anakubaliana na Kamishna wa Kazi kuwa aliwasilisha madai haya katika sheria inayotumika na siyo Sheria ya Mamlaka ya Bandari.

Akijibu hoja ya nne kuhusu suala la kuhusisha PSRC. Bw. Chapa alieleza kuwa Mlalamikiwa ni Mamlaka ya Bandari kwa vile kampuni hiyo haijabinafsishwa ila ni kitengo kimoja tu cha Container ambacho kipo Dar es Salaam. alisema kuwa kiongozi wa Bandari bado yupo na anaendelea na kazi kama kawaida. Katika hali ya kukazia hoja yake hiyo. Bw. Chapa aliomba mahakama hii irejee katika maelezo yaliyotolewa na waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kuwa Kampuni za TRC na Mamlaka ya Bandari zitakodiwa kwa wawekezaji na shughuli za kuongoza zitaendelea kama kawaida..

Akijibu hoja ya tatu Bw. Chapa alikubaliana kuwa Mamlaka ya Bandari imekuwa "specified" kwa Tangazo Na. 543/97 lakini akasisitiza kuwa mamlaka hiyo haijawa mufilisi na pia shauri lao lilianza mwaka 1994 hivyo haoni sababu kwa nini wamjumuishe PSRC. Alitoa rai yake kuwa mamlaka ilikosea kuwapunguza kazi bila kufuata mkataba. Kwa kuhitimisha Bw. Chapa alieleza kuwa mamlaka bado iko hai na kwamba mahakama hii itupilie mbali hoja za pingamizi.

Naye Msomi wakili Bw. Mchome akijibu hoja hizo za Walalamikaji, alikubaliana kuwa f.8 (a) la sheria ya Mahakama ya Kazi haikuweka "Limitation" ya kuleta "enquiries". lakini akasisitizia kuwa shauri hili liko chini ya kifungu 67 ya sheria ya Mamlaka ya Bandari ambao muda wake wa kuanzisha mashauri ni miezi 12 na hivyo kufungwa na vifungu 43 na 46 vya sheria ya ukomo (The law of limitation) act, na kukifanya kifungu 67 cha Mamlaka ya Bandari ndicho kitumike kwa vile kifungu 8(a) cha Mahakama ya kazi hakina ukomo.

Kuhusu suala la Notice Msomi Wakili Bw. Mchome alieleza Walalamikaji hawakuonyesha katika maelekezo yao kama walileta notice au barua ya kuonyesha kusudio la kuleta madai yao mahakamani. Msomi wakili Bw. Mchome alikubaliana na maelezo ya Walalamikaji wote ya kuwa mamlaka ya Bandari haijabinafsishwa ila alisema kuwa imekuwa "specified" na hivyo kuifanya PSRC iwe na mamlaka ya masuala yote ya Mamlaka ya Bandari kwa kumalizia Bw. Mchome pia alikubaliana na Walalamikaji kuwa shirika bado lilikuwa linajiendesha kibiashara.

Nikianza kuchambua hoja ya kwanza. kwamba ubatili wa mgogoro huu umeletwa bila kukidhi matakwa ya fungu 67 (a) la sheria ya kuanzisha mamlaka ya Bandari Tanzania Na. 12/1977. Nakubaliana na Msomi Wakili Mchome kuwa hiyo ni sheria iliyotungwa na kupitishwa na Bunge na inayoongoza Mamlaka ya Bandari. Napenda kusema kuwa mamlaka inayo uwezo wa kibiashara na inayo pia uwezo wa kushtaki na kushtakiwa.. Kifungu hicho kinasema tu na ninanukuu:

> S 67 "where any action as other legal proceedings is commended against the Authority for any act done in persuance or execution ........................
>
> (a) the action or legal proceedings shall not be commended against the Authority until at least one month after written notice containing the particulars of the claim, and of intention to commmence the action or legal proceedings. has been served upon the General Manager by the plaintiff or his agent."

Kwa maelezo hayo hapo juu sheria hiyo imewekwa ili kuiongoza mamlaka na jinsi ya kuchukua hatua dhidi yake pindi kunapokuwa na madai na wateja wake. Msimamo wa kisheria ni kuwa migogoro yote ya uchunguzi na kikazi kati ya Mfanyakazi na Mwajiri unatawaliwa na sheria ya Usalama Kazini (security of Employment Act). Sheria hii Na. 62 ya 1964 ndiyo inayotoa miongozo na maelekezo yote yahusuyo Usalama Kazini.

Pamoja na sheria nyingine kama za Mahakama ya Kazi Na. 41 ya 1967 na marekebisho yake na siyo sheria ya Mamlaka ya Bandari ambayo imewekwa kuongoza shirika tu na ni mambo gani muhimu yanayopaswa kufuatwa.

Lakini masuala yanayohusu maslahi ya wafanyakazi sheria inayotumika ni Sheria ya Usalama Kazini (Security of Employment Act) na Employment Ordinance.

Sina budi kusema wazi kuwa Msomi Wakili Bw. Mchome amejichanganya labda kwa kuwapotosha Walalamikiwa (with due respect) katika kutumia sheria inayoongoza shirika badala ya kutumia sheria niliyotaja hapo juu ya Usalama Kazini.

Nakubaliana kabisa na maelezo ya Walalamikaji kuwa shauri hili lililetwa na sheria husika na siyo batili na hivyo kuitupilia mbali hoja ya kwanza ya pingamizi.

Katika kujadili hoja ya pili juu ya muda wa kuwasilisha shauri hili chini ya kifungu 67 (b) kuwa Walalamikaji walete madai yao ndani ya miezi 12. Kama tulivyokwishaichambua hoja ya kwanza na ya pili pia inatawaliwa na sheria ya Mahakama ya Kazi.

Kamishna ameleta uchunguzi wa mgogoro chini ya f. 8 (a) la sheria ya Mahakama ya Kazi. Chini ya sheria hii haijafafanua juu ya ukomo (Limitation) wa kuwasilisha migogoro. Kwa kukosekana huko, mahakama hutumia sheria ya ukomo (The Law of Limitation Act) ili kuziba pego (Laeuna) inayojitokeza.

Sheria hiyo ya ukomo katika kesi za mikataba ya kazi ni miaka sita (6) hivyo shauri hili kwa kutumia sheria ya ukomo bado iko ndani ya muda. Kwa mantiki hiyo basi nalo pingamizi la pili halina msingi na nalitupilia mbali.

Katika kujadili pingamizi la tatu nakubaliana na maelezo yote ya pande zote mbili kuwa Mamlaka ya Bandari ilishakuwa "specified" kwa gazeti Na. GN 543/97 ila mamlaka hiyo haijawa mufilisi chini ya Bankrupty ordinance. Mwisho kwenye pingamizi la nne ni nani anastahili kushtakiwa na kama je mamlaka ya Bandari inahusika na shauri hili na kama Walalamikaji wanayo "cause of action".

Kama tulivyokubaliana na hoja ya tatu kuwa mamlaka ya Bandari haijawa mufilisi, ni wazi basi walalamikaji wanayo "Cause of action" dhidi ya Mamlaka ya Bandari. Sitakubaliana na Walalamikaji kuwa shauri lao lilianza mwaka 1994 kwa vile hapa mahakamani tulipokea shauri hili na kulifungulia mgogoro 1999.

Kwa vile Walalamikaji wanayo haki kisheria ya kusikilizwa mgogoro wao lakini kisheria taratibu zimewekwa ili zifuatwe na hasa ikizingatiwa kuwa hakuna ubishi kwa pande zote mbili kuwa Mamlaka ya Bandari iko "Specified" kama ilivyoonyeshwa kwenye GN 543/97.

Ili kukidhi matakwa yao, PSRC ilitakiwa kujumuishwa kwenye madai yao na hasa ikizingatiwa kuwa shauri lao lililetwa hapa mahakamani 1999. Kama ilivyonukuliwa kwenye kesi ya *Employee of Kilimanjaro Hotel Ltd. VS The Kilimanjaro Hotel Co. Ltd.* na kuwasilishwa na Menejiment. Msumi, J.K. aliyakataa madai ya Wafanyakazi kwa kutoshirikisha PSRC.

Kwa sababu hizo hapo juu madai ya Walalamikaji yanatupiliwa mbali, pingamizi ya nne kwa kutofuata taratibu zilizowekwa na sheria (procedure) ili zifuatwe.

(Sgd)
C. E. R. WILLIAM,
*Naibu Mwenyekiti*

Certified true copy of the original.

B. E. NYAMUBI,
*Registrar*

19 Novemba, 2001

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 813

MGOGORO WA KIKAZI
baina ya
WILLIAM ZAYUMBA NA WENZAKE (12) - DAR ES SALAAM
na
OYSTERBAY HOTEL - DAR ES SALAAM

UAMUZI WA

William - DC

Shauri hili ni mgogoro wa uchunguzi unaowahusu Bw. William Zayumba na wenzake 12 ambao walikuwa wafanyakazi wa Oystarbey Hotel. Walalamikaji waliajiriwa kwa tarehe na kazi tofauti. Walalamikaji hawa wanadai walipunguzwa kazi tarehe 31/7/98 (kwa kielelezo P.1).

Walalamikaji hawa katika hati yao ya madai wameeleza kuwa hawafahamu ni vigezo gani vilivyotumika katika kuwapunguza kazi, licha ya hayo wanalalamika ya kuwa tawi la CHODAWU mahala pao pa kazi haikushirikishwa katika suala zima la kuwapunguza wafanyakazi wa Hotel hiyo kinyume na kifungu cha 6 (1) (8) cha Sheria ya Usalama Kazini. Vile vile Bw. William Zayumba na wengine walikuwa wajumbe katika Tawi la Wafanyakazi na kwamba walipunguzwa kazi bila mwajiri kupata kibali cha Afisa wa Kazi na hivyo kukiuka kifungu cha 8 (b) cha Sheria ya Usalama Kazini.

Aidha mwajiri baada ya kugundua kosa hilo alitoa barua nyingine za kuwarudisha kazini cha kushangaza ni kuwa waliporudishwa kazini wafanyakazi waliishia nje ya gate hadi walipopewa barua ya pili ya kupunguzwa kazi.

Katika uchunguzi huu upande wa walalamikaji walifika mashahidi watatu PW. 1, PW. 2 na PW. 3 kwa niaba ya wenzao 12 walitoa uthibitisho huo. Vile vile mashahidi hao walielezea mahakama ya kazi kuwa Tawi la CHODAWU halikushirikishwa katika kujadili idadi ya watakaopunguzwa, vigezo vitakavyotumika na mafao ya wale watakaopunguzwa, Hivyo kwenda kinyume na kifungu cha 6 (i) (g) cha Sheria ya Usalama Kazini.

Mmoja wa walalamikaji Bw. Zayumba alielezea mahakama hii kuwa baada ya kurudishwa kazini waliitwa kwenye kikao ambapo hata Chama hakikupata nafasi ya kujadili juu ya sababu za kupunguzwa kazi na wala hakukuwa na mkataba wa aina yoyote ile.

Bw. Zayumba alitoa barua ya tarehe 11/9/98 ya kuwarudisha kazini P. 2, kwa vile menejiment hawakufuata taratibu zinazotakiwa katika kuwapunguza wafanyakazi. Ilipofika tarehe 30/9/98 walipewa tena barua nyingine ya kuwapunguza wafanyakazi Exht P. 3. Bw. Zayumba alikuwa askari.

Ushahidi wa PW. 2 Said Mohamed hautofautiani sana na shahidi wa kwanza. Kwani naye alikumbwa na zoezi hili akiwa kama Staff Cooker. Katika ushahidi wake naye alitoa barua ya kupunguzwa kazi tarehe 31/5/98 kielelelzo P. 4.

Ilipofika tarehe 11/9/98 alipata barua ya kurudishwa kazini Exht P. 5 na tarehe 30/9/98 alipata barua ya kupunguzwa kazi kwa mara ya pili Exht. P. 6, PW. 2 Said anasema kuwa yeye na wenzake waliporudishwa kazini walikuwa wote wanaishia nje ya gate hawakuruhusiwa kuingia ndani PW. 2 Said alikuwa ni mjumbe wa OTTU/ CHODAWU mahala pa kazi. Alikiri katika maelezo yake kuwa hawakuzungumzia utaratibu wa kupunguzwa kazi wafanyakazi wala utaratibu wa kulipa mafao. Vilevile alikiri kutokuwepo kwa mkataba kuhusu zoezi hili.

PW. 3 Godgizel Mrema aliye ajiriwa kama Mlinzi. Naye alikumbwa na zoezi hili la upunguzwaji kazi tarehe 31/7/98 alipopata barua ya kupunguzwa kazi, Exht. P. 7. Walitoa ripoti Tawi la OTTU siku ile ile kwa vile hawakuridhika na hatua hiyo aliyoiita ya ghafla, walipewa barua za kuipeleka mbele ya Mwenyekiti wa Mkoa juu ya suala hili.

Alikiri kupata barua nyingine iliyoitwa ya kurudishwa kazini tarehe 11/9/98 Exht. P.8. Pia nayo alisema waliporudi kazini waliishia getini ila walipewa kadi kupanch tu. Hawakufanya kazi yoyote hadi tarehe 17/9/98 walipopata tena barua nyingine ya kuwapunguza kazi Exht. P. 9. PW. 3 alisema kuwa utaratibu mzima haukufuatwa.

Baada ya ushahidi huo wa upande wa walalamikaji, upande wa mlalamikiwa Oysterbay Hotel ukiongozwa na msomi wakil Bw. Balomi ulileta utetezi wake, na uliita mashahidi wawili (2) ambao ni Toto Kibusi (DW. 1) na Ally Abdallah (DW. 2).

Toto Kibusi (DW. 1) aliiambia mahakama kwamba, yeye ni Afisa Utumishi na pia ni Karani upande wa Uhasibu, tangu Oktoba, 1977. Wakati wa zoezi la kupunguza wafanyakazi kufanyika alikuwepo. Alikiri kuwa utaratibu uliofanywa mwezi Julai 1998 ulikuwa umekosewa na haukufuata sheria. alisema hata hivyo wafanyakazi hao walipokea mafao yao alitoa Exht D.1.

DW. 1 alisema kuwa baada ya kugundua kuwa taratibu hazikufuatwa, waliandika barua nyingine za kuwarudisha kazini. Baada ya hapo menejiment alisema walikaa na CHODAWU tarehe 15/9/98 alitoa minutes Exht. D.2 waliwalipa wafanyakazi hao mishahara ya Julai - Agosti na Septemba na alitoa Exht. D. 3 na D. 4 respectively.

DW .1 alisema kuwa walipata kibali cha Afisa wa Kazi kuhusu wafanyakazi waliokuwa wajumbe wa OTTU Exht. D.5. DW. 1 amesema waliandika tena barua nyingine za kuwapunguza kazi wafanyakazi. alisema kuwa sababu iliyoleteleza kufanya hivyo ni kushuka kwa biashara na walishindwa hata kuwalipa Wafanyakazi mishahara yao. Alitoa financial statement 1997/98 kielelezo D.7 kuonyesha hasara Hotel ilipata kutokana na kushuka kwa biashara .

DW. 2 Ally Abdallah aliajiriwa na Oysterbay Hotel 1988. alitoa maelezo yake kuwa alihudhuria kikao cha menejiment walichokaa na Chama cha Wafanyakazi CHODAWU tarehe 15/9/98. Alielezea waliohudhuria kikao hicho ambao ni pamoja na wajumbe wote na mwenyekiti wa mkoa, tawi, wilaya na manejiment, DW.2 alisema kuwa walichokiongelea ni kumwasa mwajiri afuate taratibu za kuwapunguza kazi, DW. 2 alitoa muhtasari wa kikao ulioandikwa na Katibu Bw. Zinu Ramadhani kielelezo D. 10. Huu ndio ulikuwa mwisho wa ushahidi kwa upande wa utetezi.

Kamishna wa Kazi aliuleta mgogoro huu wa uchunguz kwa barua yake yenye Kumb. Na. KZ/U. 10/MG/1065/6 ya tarehe 29/1/99 chini ya kifungu cha 8 (a) cha Sheria ya Mahakama ya Kazi ya Tanzania Na. 41 ya 1967 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 3/1990 na sheria Na. 2/93 ili kufanyia uchunguzi mambo yafuatayo:-

(a) kama tawi la CHODAWU ulishirikishwa katika zoezi hili.

(b) Kama utaratibu wa FILO ulitumika.

(c) Kama ulikuwepo mkataba halali/au makubaliano ya kisheria, wakati wa kufanya zoezi hilo.

(d) Masuala mengine yoyote ambayo yataiwezesha Mahakama hii kutoa uamuzi wa haki na TUZO.

Baada ya kupata muhtasari wa ushahidi toka pande zote mbili na maandishi yao ya mwisho (final submissions) toka kwa walalamikaji na walalamikiwa, suala la kwanza ambalo linapaswa lijadiliwe na kuamliwa ni jee tawi la CHODAWU halikushirikishwa na uongozi wakati wa zoezi la kuwapunguza kazi walalamikaji. Nimepata maoni ya mshauri mmoja tu Bibi Mloli (ATE) kwa maoni yake pamoja nami tumeona kuwa lalamiko hili ni la kweli. Upande wa mlalamikiwa umethibitisha kuwa kwanza walifanya zoezi bila kufuata taratibu zinazotakiwa na sheria. Pia hasa tukizingatia ushahidi wa PW 1- PW. 3 pamoja na kuwa wajumbe wa tawi la CHODAWU mahala pa kazi walipewa barua za kupunguzwa kazi P.1- P. 3. Baadaye mwajiri kugundua kuwa amefanya makosa na baada ya kupata ushauri toka Afisa wa Kazi, mwajiri aliandika barua nyingine P.4 - P.6 za kuwarudisha kazini walalamikaji. Barua au muhtasari D. 10 anaodai mlalamikiwa kuwa ulikuwa ni muhtasari wa kikao cha menejiment na CHODAWU kinatia wasiwasi hakionyeshi kama kweli kilikuwa ni kikao cha kujadili.Bw. Kibusi DW. 1 alitajwa kuhudhuria kikao hicho na alisema kuwa yeye ndiye aliyekuwa Katibu. Pia iliambatishwa inayoitwa kauli ya pamoja ya wajumbe wa Tawi na nanukuu tu sehemu.

(1) "Tarehe 15/9/98 kilifanyika kikao cha menejiment CHODAWU TAWI NA CHODAWU MKOA"

Karatasi hii ilitiwa sahihi na watu watatu (3). 1. Ally Abdallah (2) Rashidi Makusi na Ally Seif. Haina tarehe iliandikwa lini na kikao cha tarehe 15/9/98 Exht. D. 10 ina majina ya watu kumi na mmoja (11), tu wala haizungumzii haya majina ni ya nini na nini kinaongelewa. Kwa vile yametolewa majina tu.

Kwa kweli Bw. Kibusi anaonyesha wazi kuwa hata taratibu za kufanya kikao hazitambui na jinsi ya kuandika minutes za vikao pia hazifahamu.

Kuna ushahidi wa kutosha kuthibitisha ya kuwa hakukuwa na kikao kilichoshirikisha wajumbe wa Halmashauri ya Tawi CHODAWU kwani hata ushahidi unaonyesha kuwa baada ya kurudishwa kazini, wafanyakazi walibaki siku zote getini na kupanch tu hadi tarehe 15/9/98 walipoitwa kwa wanachoita kikao.

Exht. D. 10 haionyeshi wazi kikao hicho kilikuwa kinajadili nini. Kifungu cha 6 (1) (g) cha Sheria ya Usalama Kazini kiko wazi na-nukuu.
"6(1) (g) to consult with the employer concerning any impending redundancies and The application of any joint agreement on redundancies".

Katika kielelezo D. 10 ni majina tu yaliyoorodheshwa na kichwa cha habari "Kikao cha Menejiment na CHODAWU TAWI NA CHODAWU MKOA" kilichoongelewa hakikuandikwa ile karatasi nyingine ndiyo ilisainiwa na watu watatu (3) ilikuwa na kichwa cha habari "Kauli ya pamoja ya wajumbe wa Twi la OTTU/CHODAWU 1998" na kuendelea kusema kuwa "tarehe 15/9/98 kilifanyika kikao......." hicho kikaratasi haionyeshi hata iliandikwa lini.

Kwa hiyo ni wazi kwamba kifungu cha 6(1) (g) cha Sheria ya Usalama Kazini hakikufuatwa na uongozi wa Kampuni/ Hotel ya Oysterbay.

Aidha uongozi wa kampuni/Hotel ya Oysterbay unakiuka matakwa pia ya kifungu cha 8 (b) cha Sheria ya Usalama Kazini uliowapunguza kazi wajumbe wa Tawi la CHODAWU mahala pa kazi Bw. Zayumba na wenzake watatu (3) bila kupata kibali cha Afisa wa Kazi. Kibali kilipatikana tarehe 29/9/98 baada ya kuona kuwa wamekiuka utaratibu huo.

Suala la pili ni jee utaratibu wa FILO ulitumika katika kupunguza wafanyakazi hao 13. Katika kujadili suala hili nitaliunganisha pia na suala la tatu kama kulikuwa na mkataba halali kwa makubaliano ya kisheria wakati wa kufanya zoezi hili. Katika ushahidi uliotolewa mahakamani upande wa walalamikaji hawakuelezea juu ya suala la FILO. Ushahidi huo haukuelezwa pia na upande wa utetezi. Ni maoni yangu kuwa isingelikuwa rahisi kwa mwajiri kuhusisha suala hili kwa vile hata taratibu zenyewe alisha zikiuka yaani kukiuka kifungu cha 6 (1) (g) ya sheria ya Usalama Kazini Sura 537, ambacho nilikwisha zungumzia hapo juu.

Ushahidi pia umetolewa na walalamikaji kuwa hakukuwa na mkataba wowowte ule. Ushahidi huo pia unaungwa mkono na shahidi wa mwajiri DW. 1 kuwa haukuwepo mkataba wa aina yoyote. Ushahidi uliotolewa na pande zote mbili unatosha kabisa hoja hii kwamba matakwa ya Sheria ya Usalama Kazini Sura 574 fungu la 6 (1) (g) hayakutekelezwa hivyo sheria hii imekiukwa na menejiment ya Hotel ya Oysterbay.

Baada ya uchambuzi wa ushahidi huo na hoja za hadidu za rejea za Kamishna wa Kazi ambazo zimezijibu hapo juu; ni uamuzi wangu kwamba zoezi la kupunguzwa kazi wafanyakazi wa Oysterbay Hotel halikufanywa kihalali na bila kufuata sheria na taratibu zinazohusu upunguzaji wafanyakazi. Kutokana na hayo mgogoro huu wa uchunguzi, walalamikaji wamethibitisha madai yao kuwa hawakupunguzwa kihalali na naamuru warudishwe kazini mara moja. Kwa vile hawakuwa wanafanyakazi basi watalipwa mishahara toka tarehe ya uamuzi.

Uamuzi huu umetolewa leo tarehe 15 Oktoba 2001 na unakuwa TUZO ya Mahakama.

(Sgd)
C. E. R. WILLIAM,
*Naibu Mwenyekiti*

Certified true copy of the original.

13 Novemba, 2001

B. E. NYAMUBI,
*Registrar*

---

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 814

MGOGORO WA KIKAZI
baina ya
OTTU KNY. H. ALBERT & 21 OTHERS
na
1. SUKITA
2. CCM PRINTING PRESS

UAMUZI

WILLIAM, D/C

Mgogoro huu wa uchunguzi umeletwa na Kamishana wa Kazi kwa barua yenye Kumb. Na. KZ/U. 10/MG/831/7 ya tarehe 8 Julai, 1997. mgogoro huu unahusu OTTU K.n.y. H. Albert na Wenzake 21 Dhidi ya (1) Sukita (2) CCM PRINTING PRESS.

Kamishna wa Kazi aliuleta mgogoro huu chini ya kifungu Na. 8(a) cha Sheria ya Mahakama ya Kazi Na. 41 ya 1967 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 2 ya 1993.

Kamishna wa Kazi alipouleta mgogoro huu kwa ajili ya uchunguzi aliiomba Mahakama kufanyia uchunguzi mambo yafuatayo:—

(a) kama viongozi wa OTTU walifukuzwa kazi kwa kuzingatia taratibu za sheria.
(b) kama zilikuwepo sababu zozote za msingi za kuwafukuza kazi viongozi hao pamoja na wafanyakazi wengine.
(c) Masuala yoyote mengine yatakayojitokeza wakati wa kusikilizwa kwa mgogoro huu.

Kesi hii ni moja ya mashauri yaliyopangiwa kusikilizwa Dodoma kama ilivyokuwa imeamliwa na Mwenyekiti, Jaji Mwipopo ili kusogeza huduma karibu na Walalamikaji. Taarifa za kusikilizwa kesi Dodoma zilichapishwa kwenye magazeti ya Mfanyakazi na pia kwa kutuma taarifa kwa wahusika wote kama kumbukumbu za Mahakama zinavyoonyesha.

Siku y kusikiliza kesi hii upande wa Walalamikiwa hawakuwepo. Hivyo Mahakama ilichukua nafasi ya kuwapa mwongozo Waungwana Washauri wa Mahakama na sheria inasemaje. Kifungu cha 30(2) (b) cha Sheria ya Permanent Labour Tribunal (Amendment) Na. 3 ya 1990 kinasema hivi nanukuu.

30(2) "if at the time appointed for hearing of a trade dispute or matter by the court and any of the parties refuses or *fails to appear,* the court-

.....(b) if the part absent is the person representing the employer or management, may proceed to hear and determine the dispute or matter ex-parte".

Baada ya kuridhika kuwa summons zilipelekwa, hivyo Mahakama na Waungwana Washauri wa Mahakama tulikubaliana kwa pamoja kusikiliza kesi hii kwa upande mmoja (ex-parte hearing).

Shauri hili la uchunguzi lilipangwa kusikilizwa tarehe 5/9/2000 baada ya menejiment kukosekana. Shauri liliahirishwa hadi tarehe 7/9/2000 lilipoanza kusikilizwa kwa upande mmoja.

Kwa upande wa Wawalamikaji ukiongozwa na Mwakilishi wa OTTU Bw. Chamzimu, ulileta mashahidi wawili Bw. samwel Hang (PW.1) na Hosea Arbert (PW.2).

PW. 1 Hanga alitoa ushahidi wake na alieleza Mahakama kama ifuatavyo:-

Alielezea kuwa yeye na wenzake walikuwa wanafanya kazi CCM Printing Press Dodoma. Alitoa barua za Ajira za baadhi ya wafanyakazi kama kielelezo Exh.P. 1. Pia PW. 1 alitoa barua yake ya kuthibitishwa kazini kama Fundi Binding kielelezo P.2.

Wakati akiwa CCM Printing Press alikuwa mjumbe wa OTTU Kiwandani ambaye alichaguliwa 1992. Alielezea kuwa baada ya kutokea mgogoro baina ya tawi na menejiment, Mwenyekiti Hosea albert alifukuzwa kazi na pia Katibu R. S. Mingi na mjumbe Calista Massawe nao pia walifukuzwa kazi pamoja na wafanyakazi wengine.

PW. 1 aliwataja wafanyakazi wa kawaida waliofukuzwa kazi ni pamoja Barba Adolf; Veneria Kambona; Christine Ndajiro na Zakaria Masinge.

PW. 1 alisema kuwa mwajiri alitoa Fomu Na. 1-10 kwa Mwenyekiti na Wafanyakazi wa kawaida na hatimaye kuwapa barua za kufukuzwa kazi bila kuwapa nafasi ya kujitetea.

PW. 1 na wengine walipoona Mwenyekiti na wengine kufukuzwa kazi bila kupewa nafasi ya kujitetea waliamua kuwafungia viongozi nje na viongozi kuwashtaki mahakamani kesi Na. 111/95

Mahakama hiyo ilitoa uamuzi wafanyakazi wote warudishwe kazini lakini mwajiri akawachukulia hatua ya kuwasimamisha kazi watu 15 kama Exh. P.3 kinvyoonyesha. Vilevile nao wafanyakazi waliwashtaki menejiment na madai yao yalikataliwa kwa vile hawakuwa na kibali cha DPP. baada ya hapo wafanyakazi walianza hatua zao za kuwaona viongozi wa OTTU mahala pa kazi ambapo walinyimwa huduma. Walipeleka pia OTTU (W), mkoa lakini hawakusikilizwa. Hivyo suala lao kupelekwa OTTU Makao Makuu na kote huko madai yao yalikuwa kuiomba mahakama hii itengue amri/hatua ya mwajiri ya kuwasimamisha kazi na kumwamuru mwajiri awarejeshe kazini na kuwalipa haki zao zote.

Katika kujibu suala la mshauri PW. 1 alisema kuwa utaratibu wote wa kuwafukuza kazi haukufuatwa. Pia alidai kuwa mwenyekiti wa tawi alifukuzwa kazi kwa kuwatetea waliofukuzwa kazi. PW. 2 Bw. Hosea albert aliifahamisha Mahakama kuwa aliajiriwa kama Fundi wa Uchapaji (Printer) pia alichaguliwa kuwa Mwenyekit wa tawi la OTTU Kiwandani, kwa vipindi viwili. PW. 2 alielezea mahakama kuwa mnamo tarehe 6/8/94 alifukuzwa kazi mara moja baada ya kupewa Fomu Na. 1 na 10 kwa wakati mmoja.

Akifafanua juu ya fomu hizo PW. 2 alisema kuwa Fomu Na. 1 inatumika na mwajiri akitoa kusudio lake la kutoa adhabu kwa mfanyakazi. PW. 2 alisema kuwa hakuwapa nafasi ya kuleta utetezi na kuteuliwa kikao cha Halmashauri ya tawi na mwajiri ambaye ni menejiment ili kumjadili mfanyakazi mkosaji. PW. 2 anasema kuwa hii haikufanyika na badala yake kumjazia Fomu Na. 10 bila kufuata taratibu zilizowekwa na sheria na taratibu za kazi.

Pia PW. 2 aliwataja wafanyakazi waliojaziwa Fomu kuwa ni Hosea Albert (PW.2); R. Mingi aliyekuwa Katibu wa tawi, C. Ndajilo, Rehema Faraji, Venancia Kambona na Baraba Adolf. Na mwisho alisema kuwa menejiment hawakufuata utaratibu uliowekwa na sheria ya Usalama Kazini hivyo kuiomba mahakama itengue taratibu alizotumia za kutoa adhabu na kuomba Mahakama itoe amri kuwa mwajiri awalipe haki zao zote ikiwa ni pamoja na nyongeza ya mshahara; house allowance, transport allowance; meal allowance; matibabu na mwisho warudishwe kazini. Katika kujibu hoja za washauri PW. 2 alisema kuwa mwajiri aliomba kibali kwa Afisa wa Kazi kwa wajumbe wa tawi na walikataliwa. Pia alisema kuwa suala lao ni la mgogoro hivyo wao hawakuona sababu za kupeleka malalamiko yao kwa Afisa wa Kazi bali walipeleka kwa Kamishna wa Kazi.

Bw. Chamzimu kwa niaba ya Walalamikaji aliwasilisha hoja za mwisho (final submission) kuhusiana na mgogoro huu. Katika kujibu hoja kwa ajili ya Walalamikaji hoja ya kwanza; kama viongozi wa OTTU walifukuzwa kazi kwa kuzingatia taratibu za sheria. Bw. Chamzimu alisema kuwa taratibu hazikufuatwa kwa vile mwajiri hawezi kisheria kumpa mwajiriwa fomu Na. 1 na 10 kwa pamoja na hapo hapo kumpa barua ya kumfukuza kazi bila kumpa nafasi ya kujitetea. Alisema kuwa waliohusika ni pamoja na Mwenyekiti, Hosea Albert; Katibu R. Mingi na Mjumbe Calista Massawe. Bw. Chamzimu aliita kitendo hicho ni batili (void ab initio) kwa kutozingatia taratibu za utoaji fomu kama ilivyo kwenye Government Notice Na. 98 ya tarehe 19/2/1965. Kwa kutia mkazo Bw. Chamzimu aliipeleka Mahakama katika kesi ya *Management ya Hotel African Dhidi ya Juwata* Misc. Civ App. No. 10/1978, iliamriwa kwamba iwapo sheria inaelekeza jambo fulani litendwe na lisipotendwa au utaratibu fulani ufuatwe na usipofuatwa basi matendo yoyote yanayofuata baada ya hapo yanakuwa ni batili kwa kutozingatia matakwa ya sheria.

Bw. Chamzimu aliifahamisha mahakama katika maandishi yake kuwa, uongozi ulitoa Fomu Na. 1 na 10 kwa vile waliogopa kikao kikifanyika watagundulika kuwa walikiuka sheria na vile vile hawakuwa na sababu za msingi kufanya hivyo.

Vile vile Bw. Chamzimu alisema kuwa kielelezo P. 3 kilitumika kuwasimamisha kazi wafanyakazi waliobaki na kuongeza kuwa uongozi haukuwa na sababu tena ya kuwafungia waliosimamishwa kazi kwa vile walikuwa wanasubiri matokeo ya shauri Na. 250/1995 hivyo uongozi kukiuka kifungu cha 29 (3) cha sheria ya Usalama Kazini sura 574 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 1 ya 1975 nr nanukuu:

"29(3) Not withstanding the foregoing provisions of this section, an employer may suspend on half pay any employee charged with any criminal offence which is also a breach of disciplinary code, or a conviction for which is a breach of the disciplinary code, but the suspension of an employee on half pay persuant to the provisions of this section shall not extend later than the acquittal of the employee on such charge unless another such charge is pending. No employee shall be entitled to be so suspended or shall be suspended on less than half pay"

Bw. Chamzimu katika submission yake alisema kuwa wafanyakazi hawakuwa na sababu ya kujaza fomu Na. 4 ambayo ni karatasi ya rufaa kwa Afisa wa Kazi kwa vile uongozi wa mwajiri haukuzingatia sheria kama ilivyowekwa kwenye Government Notice Na. 98 ya 965 kwa vile mkataba wa ajira wa kuwafukuza kazi ulivunjwa bila sababu za msingi.

Na mwisho Bw. Chamzimu alielezea Mahakama kuwa uongozi wa kiwanda cha SUKITA Printinng Press- Dodoma haukuomba kibali toka Afisa wa Kazi kabla ya kuwafukuza kazi wajumbe wa Halmashauri ya Tawi. Kinyume na matakwa ya sheria ya Usalama Kazini kifungu Na. 8(b) ya sheria Na. 62 ya 1964. Hivyo bwana Chamzimu kwa niaba ya wafanyakazi aliiomba Mahakama hii kuwa:

(1) Mahakama itengue uamuzi wa uongozi wa Kiwanda cha CCM Printing Press - Dodoma kwa kuwafukuza viongozi wa Halmashauri ya Tawi na baadhi ya wafanyakazi bila kuzingatia taratibu na bila kuwepo sababu zozote za msingi.

(2) Mahakama iamuru kurudishwa kazini kwa Walalamikaji waliofukuzwa na kuwafungia mlango wafanyakazi waliofungiwa nje na uongozi wa SUKITA Printing Press.

(3) Uongozi wa SUKITA Printing Press - Dodoma uwalipe Walalamikaji stahili zao ikiwemo mishahara na posho zinaostahili kwa kipindi chote ambacho uongozi ulisitisha malipo hayo.

(4) Uongozi wa SUKITA Printing Press uwatambue Walalamikaji kuwa ni wafanyakazi wa kiwanda hicho cha SUKITA Printing Press- Dodoma hadi hapo ajira zao zitakapositishwa kihalali kwa kuzingatia utaratibu wa sheria za kazi zilizopo.

Katika kulichunguza shauri hili tulitakiwa na Kamishna tuchunguze kama viongozi wa OTTU walifukuzwa kazi kwa kufuata taratibu za sheria.

Kifungu cha 8 (b) cha Sheria ya Usalama Kazini Cap. 574 kinasema nanukuu:

"8(b) an employer in whose business a committee is required to be or is, established in accordance with this Act - shall not discriminate against a member of the committee on the ground of the letter's membership of the committee and, in particular and without prejudice to the generality of the foregoing, shall not terminate the employment of a member of the committee (except for breach of the Dispinary Code) without the prior approval of labour officer."

Kutokana na kifungu hicho hapo juu na pia kwa kuzingatia kuwa ushahidi uliotolewa ulikuwa wa upande mmoja vile vile mahakama pia inazingatia kifungu cha 8(b) kilichotajwa hapo juu. Mwajiri angelionyesha hata bidii yake ya kutaka kupata kibali toka kwa Afisa wa Kazi. Hivyo hapa kuna makundi mawili ya wafanyakazi waliofukuzwa kazi na waliosimamishwa kazi. Vielelezo vya kufukuzwa kazi havikutolewa ila barua za kusimamishwa kazi zimetolewa kama Exh. P. 3. Na hizo barua zinasema nanukuu:

Ref. SUKITA/AD/DOP/PF.H/13/79 ya tarehe 10/11/1995.

Mr Samweli M. Hanga,
Print Finisher,
S.L.P. 1763,
DODOMA.

Ndugu,

Yah: KUSIMAMISHWA KAZI

kutokana na kesi ya jinai Na. 250 ya 1995 inayokukabili dhidi ya Mwajiri wako, Menejiment inakusimamisha kazi mara moja kufuatia section 29 subsection 3 ya Sheria ya Usalama Kazini ya 1964 Cap 574 hadi shauri litakapokwisha na uongozi kuja kutafakari kosa ulilolitenda kwa mwajiri wako kutokana na kanuni za utii kazini.

wako,

CCM Printing Press Ltd.

T. R. O. Simkwayi
*AG. Chief Printer*

Nakala: Mkurugenzi Mtendaji,
SUKITA Makao Makuu,
DAR ES SALAAM.

Kama nilivyosema hapo juu kesi hii ilisilikizwa upande mmoja kwa Walalamikiwa kukosa kufika na Wakili wao na bila taarifa yoyote. Kama tulivyosema hapo juu ni kuwa viongozi wa Chama cha Wafanyakazi wanao utaratibu wao wa kuwasimamisha/kuwaachisha kazi. Kama ilivyoelekezwa

kwenye Sheria Na. 62 ya 1964 ya Usalama Kazini. Na ni wajibu wa mwajiri pia kuiarifu ofisi ya kazi na kuomba kibali lakini katika sheria hiyo pia inasema (except for breach of displinary code).

Kwa kukosa kuomba kibali mwajiri alikiuka taratibu. Mshauri mmoja pia amekubaliana kuwa mwajiri alikiuka taratibu zilizowekwa na sheria. Kwa maoni ya mshauri wa pili pia aliongezea na kusema kuwa wafanyakazi nao walikiuka taratibu za sheria kwa kuwafungia viongozi nje kinyume na taratibu chini ya kifungu IIA cha Sheria ya Kazi nanukuu:

"IIA cha nothing in this act shall authorize-

(a) *employees to take part in any act to locking in or locking out: their employers:*

Kifungu hiki kwa tafsiri ni kuwa kinazuia mfanyakazi kumfungia mwajiri nje au ndani na neno "shall" ni lazima kwa hiyo kwa kufanya hivyo ni kukiuka taratibu zilizowekwa na sheria.

Kwa kuungana na washauri wa mahakama kwa pamoja tumeona na kuchunguza kuwa pande zote zimekiuka taratibu za sheria.

Katika kuchunguza hoja ya pili inasema kwamba kama zilikuwepo sababu zozote za msingi za kuwafukuza kazi viongozi hao pamoja na wafanyakazi wengine. Katika kipengele hicho pia na ushahidi uliotolewa inaonyesha kuwa viongozi na wafanyakazi wengine walipewa Fomu Na. 1 na 10 kwa wakati mmoja.Fomu hizo hazikutolewa mahakamani kama kielelezo ili mahakama ione, bali ni maelezo tu ya shahidi kuwa alijaziwa Fomu Na. 1 na 10 kwa wakati mmoja na hata hiyo barua ya kufukuzwa kazi hakuitoa ili mahakama ione ni sababu zipi zilizofanya mwajiri awafukuze kazi. Inaonyesha kuwa baada ya kupewa Fomu Na. 1 na 10 na barua ya kufukuzwa kazi mfanyakazi alinyimwa haki yake kikatiba ya kujitetea.

Pamoja na hayo SUKITA iliwafukuza kazi viongozi bila kupata kibali cha Afisa wa Kazi. Hata kama walikuwa na sababu nzito sana za kuwafukuza kazi, mwajiri alitakiwa afuate taratibu zilizowekwa na sheria ya kazi hivyo kukiuka matakwa ya kifungu cha 8(b) cha Sheria ya Usalama Kazini. Miongoni mwa waliofukuzwa kazi walikuwemo wajumbe watatu wa halmashauri ya tawi la OTTU la SUKITA. Wajumbe hao ni Hosea Albert, Mwenyekiti wa tawi, R. S. Mingi Katibu wa Tawi na C. Massawe Mjumbe. Uongozi haukuomba kibali inavyoonyesha na ndiyo sababu ikatoa Fomu Na. 1 na 10.

Pia katika kesi ya *Bw. Mwita Zebron na Wenzake dhidi ya SUKITA Na. 25* ya 1996 Mhe. Mlelwa, Naibu Mwenyekiti kama alivyokuwa alisema nanukuu:

"..... Sheria ya Usalama Kazini inamtaka mwajiri kupata kibali cha Afisa wa Kazi akitaka kumwachisha kazi mjumbe wa halmashauri ya Tawi la Chama cha Wafanyakazi mahali pa kazi kwa sababu maofisa wa kazi ni wasimamizi wa uchaguzi wa wajumbe wa halmashauri za matawi ya vyama vya wafanyakazi katika maeneo yao ya mamlaka za kazi (in their areas of jurisdiction), kazi hiyo wanaifanya wakisaidiana na viongozi wa vyama vya wafanyakazi wa wilaya ngazi za wilaya. Hivyo basi ili kuhakikisha..........mwajiri anapaswa aombe kibali kwa Afisa wa Kazi kwa kumwachisha kazi mjumbe wa halmashauri wa tawi la chama cha wafanyakazi."

Hivyo kuwafukuza kazi wajumbe watatu (3) wa halmashauri ya Tawi la OTTU la SUKITA mwajiri alikiuka matakwa ya kifungu cha 8(b) cha Sheria ya Usalama Kazini na pia uongozi ulipotoka kisheria ulipowafukuza kazi wajumbe watatu wa halmashauri ya Tawi la OTTU bila kufuata matakwa ya kifungu cha 8(b) cha Sheria ya Usalama Kazini, kwa hiyo basi naamuru wajumbe hao Bw. Hosea Albert, T. Mingi na C. Massawe warudishwe kazini tangu tarehe yao ya kufukuzwa kazi bila kupoteza stahili zao za utumishi. Kama SUKITA ina nia bado ya kuwaachisha kazi basi wafuate utaratibu wa kisheria katika kufanya hivyo.

Kuhusu wafanyakazi waliosimamishwa kazi tarehe 10.11.1995 barua zao zinasema kama nilivyonukuu hapo juu... hadi shauri litakapokwisha Na. 250/1995. Kufuatana na Exht. P. 4 kesi ilikwisha tarehe 7/12/1995 na nanukuu:

"*Order*: Charge against the accused is withdrawn under section 98 (a) and the accused are acquitted as prayed.

(Sgd)

D. M. LESSA - SDM

7 Desemba, 95

Kwa kufuata kifungu Na 29 (2) na nanukuu:

"29 (2) where an employee has been acquitted of a criminal charge no proceedings for the imposition of the disciplinary penalties of summary dismissal or deduction from wages under this Act *shall* be instituted against him for a breach of the disciplinary code which is substantially the same as the criminal charge or which he was acquitted".

Kufuatana na kifungu hicho hapo juu ni wazi kuwa mwajiri alipaswa kwanza awarejeshe kazini halafu afuate taratibu za kuwaachisha kazi. Badala yake hakuna kilichoendelea hadi leo.

Kufuatana na maoni ya Washauri naye pia aliona kuwa uongozi wa SUKITA Printing Press ulikiuka taratibu zilizowekwa na sheria kwa kifungu cha 29 (3) Sura ya 574 na kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 1 ya 1975, kwa pamoja tumeona kuwa kifungu hiki kilikiukwa na uongozi kwani kifungu kinasema na nanukuu:

"29 (30 Notwithstanding the foregoing provisions of this Section, an employer may suspend without pay any employee (including an employee already suspended or half pay) charged with criminal offence which is also a breach of disciplinary code, or a conviction for which is a breach of the disciplinary code, but the suspension *shall* not extend later the acquitted of the employee on such charge unless other such charge is pending, No employee *shall* be entitled to be so suspended.

Kifungu hicho hapo juu na Exht. P. 4 kinaonyesha kuwa washtakiwa kumi na tatu (13) waliachiwa tarehe 7/12/95. Ilikuwa ni wajibu wa mwajiri kumrudisha kwanza kazini mwajiri na kama alikuwa na sababu zingine za kumwachisha kazi basi taratibu zingelifuata.

Hata hivyo baada ya kuwasimamisha kazi pia hajawapa barua ya kuwaachisha kazi. Hivyo pamoja na maoni ya Washauri tumeona kuwa wafanyakazi hao (13) waliosimamishwa kazi mwaka 1995 bado ni wafanyakazi halali kwa vile hawajapewa barua za kuwaachisha wala kuwafukuza kazi.

Hivyo basi katika suala zima la kuwasimamisha kazi wafanyakazi 13 wa SUKITA uongozi wa shirika hilo ulikiuka utaratibu wa kuwaacha wafanyakazi wakining'inia na barua zao za kusimamishwa kazi na bila kujua hatima yao. Ndiyo kusema kusimamishwa kazi wafanyakazi hao kulikiuka matakwa ya kifungu 29(2) cha Sheria ya Usalama Kazini.

Tukirudi nyuma pia nao wafanyakazi walikiuka taratibu zilizowekwa na Sheria ya Kazi kutowafungia viongozi bila kuwa na kibali.

Nimezingatia kwa uundaji hoja za mwisho zilizoletwa na Bw. Chamzimu wa OTTU kwa upande wa Walalamikaji na maombi yake katika Mahakama hii. Hata hivyo kutokana na hadidu za rejea alizoleta Kamishna wa Kazi kwa ajili ya uchunguzi, ingawa ushahidi ni wa upande mmoja umejenga sana upande wa Walalamikaji lakini kwa vile walisimamishwa kazi toka Novemba 1995 hakuna kazi waliyokuwa wakimfanyia mwajiri, pamoja na madai yao kuwa na msingi. Hivyo mwajiri namwamuru awalipe mishahara ya miezi kumi na mbili tu (12) wafanyakazi (13) waliosimamishwa kazi.

Na kwa wafanyakazi watatu yaani Barba Adolf C. Ndajilo na Rehema Faraji kufukuzwa kazi kwao kulikuwa halali na hivyo malalamiko yao hayana msingi na ninayatupilia mbali.

Uamuzi huu umetolewa leo tarehe 24, Oktoba, 2000 na unakuwa ni TUZO ya Mahakama.

(Sgd)
C. E. R. William, D/C

**Certified true copy of the original.**

B. E. Nyamubi,
14 Novemba, 2000 *Registrar*

---

Taarifa ya Kawaida Na. 815

UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI
(Katika Mahakama Kuu ya Tanzania Dar es Salaam)
Shauri Na. 28 la Mwaka 2001
*Maombi ya barua za Usimamizi wa Mirathi ya Ahmed s. Akrabi, Marehemu*
na
Salum Saleh, Muombaji

TAARIFA YA KAWAIDA
(Kanuni ya 75)

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri hayo katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua za usimamiaji wa Mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu/Waombaji waliotajwa hapa juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 2 mwezi wa Februari, mwaka 2002.

Imewasilishwa Dar es Salaam leo tarehe 23 mwezi wa Novemba mwaka 2001.

*Naibu Msajili Mwandamizi*